BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika,

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena tukiwa hai na wazima wa afya ambayo ni neema kubwa kwetu kwa lengo la kujadili bajeti mwaka 2021/2022 kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika,

Pia napenda kukushukuru wewe binafsi kuweza kunipatia nafasi hii mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati juu ya utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika,

Aidha napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Maji, Nishati na Madini inayoongozwa na Mhe Suleiman Masoud Makame na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dr. Mngereza Mzee Miraji kwa utendaji mzuri wa kazi zao na ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Hata hivyo, napenda kuishukuru Ofisi hii kuweza

kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu bajeti ya Wizara yao kwa mwaka 2021/2022 kwa umahiri mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, pongezi za dhati ziende kwa wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanayofanya na ushirikiano wanaouonesha kwa pamoja katika kutekeleza majukumu ya kazi zao kwa mda wote bila kujali naomba sasa niwatambue wajumbe wanaounda kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yahya Rashid Abdulla — Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Foum Mussa — Mjumbe
4. Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed — Mjumbe
5. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe — Mjumbe
6. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Mjumbe
7. Mhe. Rukia Omar Ramadhan — Mjumbe

Aidha, Kamati hii ina makatibu wawili ambao wanaiwezesha kutekeleza majukumu yake kitaalamu na kiufanisi zaidi. Makatibu hao ni:-

1. Ndg. Rahma Kombo Mgeni, na
2. Ndg. Ali Alawy Ali.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo naomba sasa kutoa maoni ya kamati kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa bajeti hii kwa mwaka 2021/2022 kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Maji, Nishati na Madini yenye fungu N03 ina jumla ya program kuu tatu (3) na program ndogo sita (6) ambazo zinajumuisha idara na taasisi mbali mbali ziliopo chini ya Wizara ambapo baadhi ya idara zimerithi bajeti kutoka wizara ya zamani.

**Mheshimiwa Spika,**

Utekelezaji wa Program hizi umezingatia Mipango Mikuu ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2020 – 2025, Mpango wa kukuza uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)2025, Ahadi zilizotolewa na Mhe Rais Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi cha kampeni za Uchaguzi, Hutuba ya Mheshimiwa Rais katika ufunguzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi na Maagizo ya Utendaji kwa Mawaziri na Makatibu Wakuu ambayo huyatoa katika Hotuba zake toafuti.

**Mheshimiwa Spika,**

***Kupitia program kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji:*** Kamati inapongeza Mamlaka ya Maji ZAWA kwa jtihada zao wanazozifanya kwa kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwa Unguja na Pemba licha ya changamoto zilizopo kwa baadhi ya maeneo. Hata hivyo, mbali na jitihada hizo kamati inashauri Mamlaka kuhakikisha suala la upatikanaji wa maji safi na salama ni la lazima kwani hakuna mbadala wa maji.

Hivyo basi, Kamati inaitaka Mamlaka ihakikishe inatatua changamoto zote ikiwemo kuziba mivujo kwa ajili ya kuzuia upotevu wa maji, kubadilisha mabomba chakavu na kuweka yenye ubora na yenye ukubwa unaotosheleza kwa mahitaji ya watumiaji  nakuvifanyia usafi visima vya maji kwa Unguja na Pemba ili huduma ya maji ipatikane na kuwaondoshea usumbufu wananchi. Ni

wazi kuwa iwapo huduma ya maji itapatikana kwa ukamilifu basi hata makusanyo nayo yataongezeka.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati inashauri Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia bajeti hii kuhakikisha inaendelea kuhifadhi vianzio vya maji kwa kuvijengea uzio ili kuepusha uharibifu pamoja na uvamizi unaoendelea katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba. Lakini pia Mamlaka kupitia Wizara ya Ardhi ihakikishe inafatilia upatikanaji wa hatimiliki kwa maeneo yaliyobakia ya visima na vyanzo vya maji ili kuzuia uvamizi unaoendelea, ambapo kwa sasa Mamlaka imeweza kuyapatia hatimiliki maeneo 67 tu kati ya maeneo 302, idadi hii ni ndogo sana hasa kwa kuwa uvamizi wa maeneo yake umekuwa mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**,

Kamati inashauri Taasisi za Serikali na Watu binafsi pamoja na wananchi wahakikishe wanafuata utaratibu wa malipo ya huduma ya maji kwa wakati na kuondokana na tabia yakulimbikiza madeni ambayo yanaikwaza Mamlaka katika ukusanyaji wake wa mapato,kwani hadi kufikia March 2021 ZAWA inadai kwa wateja wa majumbani na Taasisi za Serikali jumla ya **Tsh Bilioni 6**. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kusimamia Taasisi zake kwa kuchangia huduma za maji kikamilifu kwani Taasisi hizi ndio watumiaji wakubwa wa huduma za maji.

**Mheshmiwa Spika,**

Hata hivyo, Kamati inaiomba Mamlaka kuhakikisha thamani ya fedha ya miradi yake (value for money) inazingatiwa pamoja na kiwango bora cha miradi hiyo ili huduma ya maji ipatikane kwa uhakika kwani kutozingatia thamani halisi ya fedha inayotumika katika miradi hiyo kunaifanya jamii kutokuwa na imani katika utekelezaji wa kazi zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia, inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Ujenzi,Mawasiliano na Uchukuzi wakati wa ujenzi wa barabara zetu kuhakikisha suala la kurejesha miundombinu ya maji limesimamiwa kikamilifu na kuacha tabia ya kukata miundombinu hiyo na baadae kuiacha bila kuirejesha kwa wakati hali ambayo inarejesha nyuma jitihada za Serikali za kuwapatia huduma tofauti za kiuchumi na kijamii, hivyo kuwapa shida wananchi katika kuipata huduma hiyo muhimu ya maji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inatoa wito kwa wananchi wote wenye tabia ya kuharibu miundombinu ya maji na kusababisha kukosekana kwa huduma hii muhimu kuacha mara moja tabia hiyo kwani inapelekea hasara kwa Serikali na usumbufu kwa wananchi katika suala zima la upatikanaji wa maji. Aidha, kamati inaitaka Mamlaka kuwachukulia hatua za kisheria kwa wale wote wanaoharibu miundombinu ya maji mara tu wanapowagundua kwa kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Hata hivyo, kamati inawashajihisha wananchi kuwa walinzi katika maeneo yao na kutoa taarifa pale ambapo kunatokea uharibifu katika vyanzo au miundombinu ya maji kwa vyombo husika.

**Mheshimiwa Spika,**

***Kupitia program kuu ya usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini*** ambayo imepangiwa jumla ya **TSH. Bilioni 14, 478, 965,000** katika utekelezaji wake. Kamati inatoa pongezi kwa Wizara kwa hatua walizochukua za kufanya mazungumzo na wawekezaji wa nishati mbadala na kampuni mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kumekuwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika ambao utawaondolea usumbufu wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inatoa pongezi kwa wizara kupitia Shirika la Umeme Zanzibar kwa kufanikisha punguzo la bei ya kuunganisha umeme kwa wananchi kwa wastan wa asilimia 50. Mbali na punguzo hilo,Kamati inashauri Shirika kuongeza nguvu ya kuboresha huduma za umeme katika maeneo yote ya Unguja na Pemba kama vile; kubadilisha nguzo mbovu ambazo zimekua zikileta athari zinapoanguka na kuweka transfoma zenye uwezo mkubwa kwa mujibu wa mahitaji ya eneo husika ili kuepuka hasara zinazotokea kwa watumiaji ikiwemo ya kukatika umeme mara kwa mara pamoja na kadhia ya umeme kuwa mdogo kwenye maeneo mengi ya Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapongeza kwa dhati kabisa juhudi zinazofanywa na Shirika la Umeme Zanzaibar kwa namna wanavyokabiliana na changamoto mbali mbali katika kuhakikisha huduma za umeme zimepatikana kila siku katika jamii. Hata hivyo, kwakuwa uendeshaji wa huduma za umeme ni gharama kubwa na zinahitaji wataalamu wakutosha katika kufanikisha maendeleo yake.

Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya madeni ambayo yanapelekea Shirika kishindwa kutekeleza mipango yake ipasavyo kutokana na kudai kiwango kikubwa cha fedha ambapo wastani wa **TSH. Bilioni 42.4** kutoka Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzabar na Taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinadaiwa wastani wa **Tsh. Bilioni 2.06** hadi kufikia mwezi wa March 2021.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini kusimamia Taasisi zote ambazo zinahusika na madeni haya kwa kutengeneza utaratibu maalum ambao utasaidia pande zote mbili kuyalipa madeni haya kwa wakati. Pia, kwa zile Taasisi za Muungano kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu

zilivyo ili kusudi kusaidia utekelezaji wa Shirika hili ambalo ndio tegemeo kubwa kwa huduma za nishati hapa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika suala zima la sekta ya Madini, Kamati inaiopongeza Wizara kuandaa utaratibu mpya wa upatikanaji wa mchanga ambapo kwa sasa wamiliki wa mashamba yanayotoa huduma hiyo ya uchimbaji mchanga wananufaika moja kwa moja kupitia makusanyo yanayopatikana katika uchimbaji huo. Pia, tunaipongeza Idara kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji mara tu baada ya sekta hii kuletwa katika Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, Kamati kupitia suala hili inaishauri Wizara kuendea kufatilia urudishaji wa ardhi baada ya kuchimbwa ili kuepuka athari za kimazingira na kuweka maeneo kuwa salama kwani baadhi yao yanakua karibu na jamii.Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuliangalia kwa kina suala la uagiziaji mchanga kutoka nje ya Nchi ili lisije likaleta athari za kibaiolojia.

Vile vile, Kamati inaiomba Wizara ya Fedha kuhakikisha mapato yanayopatikana kwenye Madini ya Mchanga na sehemu ya asilimia 46 kurejeshwa Idara ya Madini linafanyika kwa mujibu wa taratibu husika na kwa wakati ili kufanikisha malengo ya Idara hii.

**Mheshimiwa Spika,**

***Kupitia program kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara.*** Kamati inaunga mkono malengo yaliyowekwa kupitia program hii kwa mwaka 2021/2022 na inaomba Serikali iwaidhinishie jumla ya **Tsh.1,594,479,000** kwa ajili ya kuweza kutekeleza mipango yao na kuweza kuleta mabadiliko kwa manufaa ya nchi yetu. Kamati inaitaka Wizara kuzidi kuzisimamia Taasisi zake zenye kutoa huduma kwa jamii ili kuhakikisha huduma wanazotoa ni bora na zinakidhi mahitaji kwa mujibu wa maeneo husika.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaitaka Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhakikisha wanajitahidi katika ukusanyaji wa mapato kupitia vianzio vyao vilivyopo ili kuweza kuongeza ufanisi katika kazi zao na mapato kwa Serikali ambapo kwa mwaka huu wamepangiwa kukusanya jumla ya **Tsh.7,743,262,000.**

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, kupitia Bajeti hii ya 2021/2022 Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kukamilisha malengo yao kwa mwaka huu kwa maendeleo ya wananchi na Nchi kwa ujumla. Kwani, kucheleweshwa kwa fedha za matumizi mengineyo kunapelekea watumishi kutolipwa stahiki zao mbali mbali wakati ni haki zao kisheria.

Hata hivyo, Kamati inashauri kuwepo kwa mafungu maalum ya kuwasomeshea watumishi wake ili kuwajenga kiuwezo badala ya kutegemea fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa kusomesha watumishi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, ili kufikiwa malengo waliyojipangia katika utekelezaji wa majukumu yao;Wizara ya Maji, Nishati na Madini na kwa niaba ya kamati hii tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waichangie na wairidhie Bajeti hii na hatimae wapitishiwe mapato na matumizi ya fedha zote zilizopangwa kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

*Kwa niaba ya Kamati yangu* ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

…………….……………………..

(Hudhaima Mbarak Tahir)

Makamu Mwenyekiti,

KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI

BARAZA LA WAWAKILISHI,

<u>ZANZIBAR</u>